**Mimi ni nani katika Kristo.**

**Lakini katika Kristo, nyinyi ambao kwanza mlikuwa mbali mumevutwa karibukwa damu ya Kristo.**

Waefeso 2:13.

Baadhi ya yale mambo yakwanza ulifunzwa utotoni ni jina lako. Baba yako wa mbiguni pia anajua umuhimu wa utambulisho wako- ndiposa amekufanya kiumbe kipia ndani yake wakati ulimpokea yesu Kristo kama mbwana (1wakorintho 5:17). Mungu anataka wewe ujione kama mmoja(kwa umoja, katika makubaliano) na yeye, ili kwa ushindi uwavutie watu wengi kwake.

Sababu ya kuishi kwako katika kushindwa, kukata tama ama kushushika, ni kwa sababu haujajiona kwa macho ya mungu. Umejitazama katika kioo cha maisha ya kale, kile ambacho watu wanasema kukuhusu, uongo ambao shetani amekunonezea nawe ukaamini. Sasa ni wakati wakujitazama kupitia kwa kioo cha neno la mungu, biblia.

Warumi 12:2 inakuonyesha jinsi ya kufanya haya. (yasema: "usijifananishe na mtindo wa ulimwengu, lakini ihuishe nia yako kwa.")unapojilishi kila siku kwa neno, atakuonyesha kwa uwazi wewe ni nani kama anayemuamini. Utawacha kujiona katika kioo cha kale, na uongo ambao uliamini utabadilishwa na maono ya kweli ya mungu kuhusu wewe.

Nakala hizi zimepeanwa kwako kama chanzo cha uhuru wako. Unapo somanistari hizi, tunakuhimiza ufungue biblia yako na ujionee kile mungu ameandika kukuhusu. Lakini tafadhali usikomee hapo.kiri kila ahadi kwa sauti,changanya na imani, kisha upokee ufunuo, kwamba, wewe ni yule mungu anasema na kwamba uko na kile Mungu anasema uko nacho.

Maneno ya mungu ya na nguvu kushinda uongo wa shetani, utahisi nguvu zake kubadilisha maisha yako mara tu utakapo kubaliana na kile anasema. Maombi yetu kwako ni kwamba utaishi maisha yako "NDANI YA KRISTO,"ukiwa na uhakika wa upendo wake na utambulisho wako ndani yake, kwamba utajiona kupitia kwa macho yake na kuangaza utukufu wake kwa wengine. Chukuwa wakati leo kuona na kukumbuka jinsi ulivyo katika Kristo. Mruhusu Roho Mtakatifu kukuonyesha huu ukweli, na maisha yako hayatasalia kawaida.

**JE UMEMPOKEA YESU KAMA BWANA NA MWOKOZI.**

Kama si hivyo, natufanye sasa. Biblia yasema katika warumi 10:9-10 kwamba nikikiri na kinywa changu kwamba yesu ni bwana na nikiri kwa moyo kwamba Mungu alimfufua kutoka kwa wafu nitaokoka. Ninaamini kwamba yesu ni mwanao na alikufa kwa ajili ya dhambi zangu, na ulimfufua kwa mauti kwa ajili ya wokovu wangu. Bwana Yesu, ninakuuliza unisamehe dhambi zangu zote na uje ndani ya moyo na maisha yangu uwe mwokozi, bwana na mwokozi. Amen.

**BABA WA MBIGUNI AMESEME NAMI NAAMINI:**

Mimi ni chuvi ya dunia…mathayo 5:13

Ninapo ongea kulingana na neno na mapenzi ya Mungu mbingu huwajibika… marko 11:23-24

Ninauliza na ninapokea; ninatafuta na ninapata; ninabisha nakufunguliwa… luka 11:9-10

Ninauzima wa milele… yohana 3:36, nimepitishwa kutoka kwa mauti na uhai… 5:24 kutoka kwa vilindi via moyo wangu kunatiririka maji ya uzima… yohana 7:38 ukweli umeni weka huru… yohana 8:31-32 nikiuliza kile mungu amekuahidi, kwa jina la yesu, atatenda… yohana 14:14 niko kwa Kristo, na Kristo yu ndani yangu… yohana 14:20 nina amani… yohana 14:27 nimependwa na Yesu… yohana 15:9 nimependwa na baba… yohana 16:27 mimi ni wa mungu, mimi ni wake… yohana 17:9 nimelindwa kutokana na muovu… yohana 17:15 nimetakaswa kwa ukwel wa neon la mungu… yohana 17:17 nimetumwa ulimwenguni… yohana 17:18 nina utukufu wa Mungu… yohana 17:22 niko kwa Kristo na ninapendwa na baba… yohana 17:23

Nimesamehewa dhambi kupitia kwa Kristo… Matendo ya mitume 13:38 niko huru kutoka kwa vitu vyote… Matendo ya mitume 13:39.

Niko kati ya walioitwa na Yesu Kristo… warumi 1:6 nimpedwa wa Mungu, mtume… warumi 1:7 nimefanywa mwenye haki kwa imani, niko na amani na Mungu kupitia kwa bwana wetu Yesu Kristo… warumi 5:1 nina neema kwa imani… warumi 5:2 nina uvumilivu, uadilifu na tumaini… warumi 5:3,4 upendo wa Mungu umemwagwa kwa roho yangu kupitia kwa kifo cha Yesu… warumi 5:5 nimeokoka kwa maisha yake… warumi 5:10b ninatawala maishani kupitia kwa Yule Kristo Yesu… warumi 5:17 nimafanywa mwenye haki hupitia kwa utiivu wa Kristo… warumi 5:19 nimekufa kwa dhambi… warumi 6:2 nimebatizwa kwa mauti ya Kristo… warumi 6:3 nimeinuliwa na Kristo kutoka kwa mauti ili nitembee kwa uupia wa maisha… warumi 6:4 nimesulubishwa na Kristo… warumi 6:6a mimi siko chini ya ya dhambi… warumi 6:6b nimekufa kwa dhambi na ni hai kwa Mungu kupitia Kristo Yesu… warumi 6:11 siko chini ya sheria, bali chini ya neema… warumi 6:14 ni mateka wa haki… warumi 6:18 si dhihakiwi… warumi 8:1 ni huru kutokana na sheria ya dhambi na mauti… warumi 8:2 nina maisha kupitia Roho wake akaae ndani yangu…

warumi 8:11 ni mwana wa Mungu… warumi 8:16 nimrithi wa Mungu na mrithi pamoja na Kristo… warumi 8:17 mambo yote yatendeka kwa wema… warumi 8:28 nimefanywa haki na kutukuzwa… warumi 8:30 nina kipimo cha imani… warumi 12:3 nimepewa vipawa… warumi 12:6 nife au nisife, niwa bwana… warumi 14:8 nimejazwa na wema na maarifa, kama ilivyo peanwa na Roho Mtakatifu… warumi 15:14

Mimi ni mtakatifu aliyetkaswa katika Yesu Kristo… 1wakorintho 1:2 nimepewa neema ya Mungu katika Kristo Yesu…1wakorintho 1:4 ndani yake nimeridhishwa kwa kila njia…1wakorintho 1:5 sipungukiwi kwa kipawa chochote cha kiroho…1wakorintho 1:7 nimeitwa katika ushiriki na Yesu Kristo Bwana wangu…1wakorintho 1:9 ni kwa Kristo Yesu anipaye hekima, haki, utakaso na urejesho…1wakorintho 1:30 nimepewa Roho wa Mungu niweze kuelewa kile Mungu amepeana bure…1wakorintho 2:12 niko na nia ya Kristo… 1wakorintho 2:16 mimi ni mtenda kazi pamoja na Kristo, mimi ni kiwanja cha Mungu, njengo la Mungu… 1wakorintho 3:9 mimi ni hekalu ambalo anakaa Roho wa Mungu…1wakorintho 3:16 mimi ni hekalu takatifu la Mungu… 1wakorintho 3:17 vitu vyote ni vyangu, kwa sababu mimi ni wa Kristo…1wakorintho 3:21,22 nina Roho moja na Kristo…1wakorintho 6:17 mwili wangu ni hekalu la Roho mtakatifu aliye ndani yangu…1wakorintho 6:19 nimenunuliwa kwa garama, ninamuheshimu Mungu na mwili wangu…1wakorintho 6:20 ni mateka wa Kristo.. 1wakorintho 7:22 nitainuliwa kutoka kwa wafu…1wakorintho 15:52 nitavalia mwili wa milele…1wakorintho 15:53

Nimefarijika na Mungu, hivyo nina wa fariji wengine…2wakorintho 1:4  nimekobilewa kutoka kwa mauti…2wakorintho 1:10 amenipaka na kuweka muhuri wa umiliki kwangu…2wakorintho 1:22 mimi ni marashi mazuri ya ufahamu wa Kristo…2wakorintho 2:14 ni manukato ya Kristo kwa Mungu kwa waliookolewa na wasiookoka…2wakorintho 2:15 mimi ni barua ya Kristo…2wakorintho 3:3 ni muhuduma wa agano jipya la Roho wa maisha…2wakorintho 3:6 palipo Roho wa Mungu kuna uhuru…2wakorintho 3:17 nina badilishwa kwa mfano wa bwana nikiongezeka kwa utukufu wa Mungu…2wakorintho 3:18 nimepokea rehema na sikati tama…2wakorintho 4:1 niko na Roho Mtakatifu mwilini mwangu…2wakorintho 4:7 maisha ya Yesu yanathihirishwa kwangu…2wakorintho 4:10 mtu wangu wa ndani anauishwa siku kwa siku…2wakorintho 4:16 nina nyumba ya umilele mbinguni…2wakorintho 5:1 ninaishi kwa imani wala si kwa hisia …2wakorintho 5:7 nikiumbe kipya katika Kristo yote yamepita yote nimapya…2wakorintho 5:17 nmerejeshwa kwa Mungu kupitia kwa Kristo na nimepewa huduma ya urejesho…2wakorintho 5: 18 ni balozi wa Kristo nikiwashawishi watu kumrejelea Mungu…2wakorintho 5:20 mimi ni mwenye haki wa Mungu katika Kristo Yesu…2wakorintho 5:21 nina neema kutoka kwa Mungu kwa ajili ya kazi njema…2wakorintho 9:8 mimi ni wa Kristo …2wakorintho 10:7 yesu Kristo yu ndani yangu …2wakorintho 13:5

Nimesulubiwa na Kristo. Si mimi aishiye bali Kristo aishiye ndani yangu, maisha ninayoishi naishi kwa imani…wagalati 2:20 mimi ni mwana wa Mungu kwa imani kupitia Kristo Yesu…wagalati 3:26 ni mmoja ndani ya Kristo Yesu na watakatifu wote…wagalati 3:28 mimi ni wa Kristo. Ni mrithi kulingana na ahadi…wagalati 3:29 mimi ni mwana wa Mungu …wagalati 4:6 mimi si mateka lakini mwana, mrithi kupitia kwa Kristo …wagalati 4:7 nina tunda la Roho ambalo ni upendo, furaha, amani, subira, ukarimu, wema, uaminifu, upole, kiasi …wagalati 5:22-23.

Nina neema na amani…waefeso 1:2 nimeberikiwa na Baraka zote za kiroho katika Kristo…waefeso 1:3 nimeteuliwa ndani yake …waefeso 1:4a nimtakatifu sinalawamu bila zake …waefeso 1:4b ni mwana wa Mungu kupitia Kristo …waefeso 1:5 nimekubalikwa kwa wapendwa …waefeso 1:6 nina ukombozi na msamaha …waefeso 1:7 nimepokea urithi …waefeso 1:11 nimewekewa muhuri wa Roho mtakatifu …waefeso 1:13 nimewekewa muhuri na Kristo kwa mbingu …waefeso 1:20 nina kila kitu chini ya miguu yangu …waefeso 1:22 napendwa na Mungu …waefeso 2:4 nimefanya hai na Kristo pamoja na Kristo …waefeso 2:5 nimefufuliwa na yeye na kuketi nay eye mahali pa juu kwa Kristo Yesu …waefeso 2:6 nimeokolewa kwa neema kupitia kwa imani- kipawa cha Mungu …waefeso 2:8 mimi ni kazi yake; nimeubwa kwa kristo Yesu kwa ajali ya kazi nzuri …waefeso 2:10 nime letwa karibu na Mungu kwa damu ya Kristo …waefeso 13:2  Kristo ni nguvu zangu …waefeso 2:14 kupitia Kristo nimetabulika katika Roho mmoja kwa baba. …waefeso 2:18 si mgeni bali ni mwenyenji na watakatifu …waefeso 2:19a ni mrithi kwa mwili wa Kristo …waefeso 3:6a ni mshirika wa ahadi katika Kristo Yesu …waefeso 3:6b katika Kristo na kupitia imani, tuna ujasiri wa kuumfikia Mungu …waefeso 3:12nimetiwa nguvu kipitia roho wake kwa mutu wangu wa ndani…waefeso 3:16 nimetiwa mizizi na msingi kwa upendo wa Kristo…waefeso 3:17 nIko na chemichemi ya nguvu ndani yangu ambayo inaweza kunisababisha kutenda zaidi ya ninavyo uliza ama kuwaza…waefeso 3:20 nimepewa neema…waefeso 4:7 navalia nafsi mpya,kwa mfano wa Mungu,nimeumbwa kwa haki na utakatifu…waefeso 4:24 nimesamehewa nab ado nasamehe wengine…waefeso 4:32

Ninaujasiri kuwa Yule aliye anzisha kazi njema ndani yangu atikamilisha hadi siku ya Kristo Yesu …wafilipi 1:6 nimejazwa na matunda ya haki kupitia kwa Yesu Kristo …wafilipi 1:11 kwangu, kuishi ni Kristo, kufa ni faida …wafilipi 1:21 Mungu anafanya kazi ndani yangu kutenda na mapenzi kwa kusudi lake njema …wafilipi 2:13 mimi ni nuru duniani …wafilipi 2:15 amni ya Mungu analinda moyo na nia yangu ninapoomba kati ya mambo yote …wafilipi 4:6,7 Ninayaweza mambo yote kupitia yeye anitiae nguvu …wafilipi 4:13 Mungu atanitwalia mahitaji yangu yo kulingana na utajiri wa utukufu wake kwa Kristo Yesu …wafilipi 4:19

Baba ameniidhinisha kushiriki kwa urithi wa watakatifu katika ufalme wake wa nuru ….wakolosai 1:12 nimekombolewa kutoka kwa nguvu za giza na kuletwa kwa ufalme wa mwana wa Mungu ….wakolosai 1:13 nina ukombozi na msamaha wa dhambi ….wakolosai 1:14 Kristo ndani yangu; tumaini la uzima ….wakolosai 1:27 nimekamilishwa ndani ya Kristo ….wakolosai 2:10 nimezikwa na Kristo katika ubatizo. Nimefufuka na yeye kwa imani ….wakolosai 2:12 nimefanywa hai pamoja na Kristo Yesu ….wakolosai 2:13a dhambi zangu na deni yangu ililipwa yote msalabani ….wakolosai 2:14 nimefufuliwa na Kristo, na, nimeweka moyo wangu kwa mambo yaliyo juu. Nimekufa(kwa mambo yangu ya mwili) maisha yangu yamefichwa na Kristo kwa Mungu ….wakolosai 3:1-3 nimevalia mtu mpya anayehuishwa kwa ufahamu kwa mfano wa muumba ….wakolosai 3:10

Nimeokolewa na (nikiamini) Yesu(alikufa msalabani kwa ajil yangu) kutokana na hukumu ijayo … 1 wathesalonike 1:10 ninafundishwa na mungu kuwapenda wengine … 1 wathesalonike 4:9 nitakutana na bwana mawinguni na kuwa naye milele … 1 wathesalonike 4:17 nimpokea wokovu kupitia (kuamini) kwa bwana wetu Yesu Kristo … 1 wathesalonike 5:9

Napendwa na Bwana, Mungu amenichangua kwa wokovu kwa utakaso tagia mwanzo kwa Roho na imani kwa ukweli … 2 wathesalonike 2:13 Mungu mwaminifu atnitia nguvu na kunilinda kutokana na Yule muovu … 2 wathesalonike 3:3 nimeitwa kwa masha ya milele … 1timotheo 6:12

Mungu hajanipa roho wa uoga, bali wa nguvu, upendo na nia timamu … 2timotheo 1:7 bwana ameniokoa na kuniitia maisha matakatifu, si kwa kazi zangu, bali ni kwa kusudi lake na neema niliyopewa na Kristo ya milele 2timotheo 1:9 nimeshawishika atakilinda kile nimemkabidhi (gudua) kwake hadi siku ile …2timotheo 1:12 Roho mtakatifu anaishi ndani yangu…2timotheo 1:14 bwaba ameniwekea taji la haki …2timotheo 4:8 amenikomboa na matendo yote ya sheria na kunitakasa kwa ajili yake mwenyewe …tito 2:14 Roho Mtakatifu amemwangwa kwangu kwa utele kupitia Yesu Kristo Mwokozi wangu …tito 3:6 nimekamilishwa na neema yake na kufanywa mrithi nikiwa na tumaini la utukufu …tito 3:7

Ufahamu wa mambo yote mema iko ndani yangu …filemoni 1:6

Malaika wametumwa kunihudumia…waebrania 1:14 vitu vyote viko chini yangu …waebrania 2:8 nimeweka mawazo yangu kwa yesu mutume na kuhani mukuu ambaye ninamkiri …waebrania 3:1 nihekalu ya Yesu Kristo …waebrania 3:6 nimefanyika mshiriki wa Kristo …waebrania 3:14 nimeingia pumziko lake …waebrania 4:3 kama Mungu amepumzika kwa kazi yake nimepumzika kwa kazi zangu …waebrania 4:10

Ninakuhani mukuu ambaye amepita mbingu …waebrania 4:14 ninakuhani mukuu ambaye anahurumika na udhaifu wangu …waebrania 4:15 ninakisongelea kitu cha enzi kwa ujasiri, ili nipokee rehema na neema kunisaidia kwa wakati wa hitaji …waebrania 4:16 nimeokoka milele, Kristo yuaishi kunifanyia uombezi …waebrania 7:25 nimrfanyika mtakatifu kupita kwa sadaka ya Yesu mara moja ikatosha …waebrania 10:10 moyo wangu umesafifishwa kutokana na nia chafu na mwili wangu kuoshwa na maji masafi …waebrania 10:22 nina wingu kuu la mashahidi wakinizunguka …waebrania 12:1 Mungu huniadhibu kwa wema wangu ili nishiriki kwa utakatifu wake …waebrania 12:10 nimepokea ufalme ambao hautingizwi, na ninmshukuru na kumuabudu Mungu …waebrania 12:28 Mungu amesema "sitakuacha." …waebrania 13:5 nimafanywa mtakatifu kupitia kwa damu ya Yesu …waebrania 13:12 Yesu amenipa vifa kwa njia yote njema kutenda mapenzi yake, kutenda dani yangu kile kinapendeza machoni pake …waebrania 13:21

Mungu kwa utele ananipa hekima nikimuliza … Yakobo 1:5 Bwana amenihaidi taji la uzima nikivumilia majaribu … yakobo 1:12

Kwa rehema zake kuu,nimezaliwa mara ya pili kwa tumaini kupitia ufufuo wa Yesu Kristo kutoka kwa mauti … 1Petero 1:3 nimepokea urithi ambao hautaisha …… 1Petero 1:4 nimelindwa na nguvu za Mungu kwa imani hadi wakati wa wokovu ambayo itayari kuhuhishwa wakati wa mwisho …… 1Petero 1:5 kwa sababu ni mtakatifu mimi ni mtakatifu … 1Petero 1:16 sikukombolewa kwa vitu viishavyo kama dhahabu na almasi lakini na damu ya dhamana ya Kristo, mwana kondoo bila lawama au kosa … 1Petero 1:18-19 nimeokoka si kwa begu iishayo bali ya milele, kupitia kwa neon liishilo la Mungu … 1Petero 1:23 ni kizazi kiteule, kuhani wa kifalme an taifa takatifu na mtu wa miliki ya Mungu ili niweze kutangaza ukamilifu wake ambaye ameniita kutoka kwa giza hadi kwa nuru yake. … 1Petero 2:9 nisehemu ya jamii ya Mungu na nimepokea rehema … 1Petero 2:10 kwa mapigo yake nimepona … 1Petero 2:24 nimefanya hai kwa roho … 1Petero 3:18 Roho wa utukufu na Mungu yu juu yangu … 1Petero 4:14

Nguvu zake za kiungu zimenipa kila kitu kulingana na maisha na uungu kupitia kwa ufahamu wake yeye atuitae kwa utukufu wake an ukamilifu …2petero 1:3 amenipa ahadi zake kuu ili kupitia kwa hizo nipate asili yake ya kiuungu nikiwa nimewachana na ufisadi wa ulimwenguni kwa tama …2petero 1:4 nimesafishwa kutoka kwa dhambi zangu za kale …2petero 1:9

Nikikiri dhambi zangu nimwaminifu na mwenye haki na atanisamehe kutokana na uovu wote …1 yohana 1:9 dhambi zangu zimesamahewa kwa jina lake …1 yohana 2:12 upako niliyo upokea kutoka kwake unasalia kwangu, na sina hitaji ya mafundisho; lakini kama vile upako wake hunifundshi na ni kweli, na kama vile umenifundisha ninasalia kwake …1 yohana 2:27 mimi ni mwana wa Mungu …1 yohana 3:2 kwa sababu nina weka ahadi zake na kufanya mambo yanayo stahili machoni pake, chochote ninauliza ninapokea kutoka kwake …1 yohana 3:22